Kaunti ya Erie
MABADILIKO YA TABIANCHI

Mpango wa Mikakati ya Jamii ya Kukabili Mabadiliko ya Tabianchi (Community Climate Action Plan)

## KITENGO CHA VIKUNDI VYA ENEO VYA KUSHUGHULIKIA MASUALA YA TABIANCHI

### Mada Muhimu

**Haki Inayohusiana na Masuala ya Tabinchi**

Imekagua Matokeo yote kwa kutumia mtazamo wa haki ili kuhakikisha kuwa usawa ndilo jambo lililolengwa.

**Ustahimilivu kutokana na Mabadiliko ya Tabianchi**

Imekagua Matokeo yote ili kuhakikisha kuwa uelezeaji wa pamoja na wa kina juu ya mada za ustahimilivu zilizopo kwenye mpango.

**Kuwasiliana Hatua Zinazochukuliwa**

Kuipa kipaumbele suala la maoni ya jamii na uwazi katika shughuli za serikali wakati wa kuandaa rasimu ya mpango.

**Upunguzaji wa Matumizi ya Rasilimali na Upunguzaji wa Uzalishaji wa Taka**
***Lengo:*** Uzalishaji na matumizi ya rasilimali kwa njia inayojali mazingira na usimamizi endelevu wa taka.

**Usafiri**
***Lengo:*** Kuunda mfumo wa usafiri wa aina mbalimbali ulio salama, wa haki na wa bei nafuu ambao unaboresha usafiri na upatikanaji, unaoondoa utegemezi wa mafuta ghafi, unaounganisha jamii, unaosaidia mnyororo wa ugavi wenye ustahimili na kupunguza utoaji wa gesi chafu za hali ya hewa (Greenhouse Gas, GHG).

**Mikakati ya Kujenga Nyumba na Vitongoji Vyenye Ustahimilivu**
***Lengo:*** Kuweka mikakati ya kujenga nyumba na vitongoji visivyotoa hewa yoyote chafu ambayo inakuza afya na kulinda wakazi kutokana na hali mbaya ya hewa.

**Ukuzaji wa Uchumi na Wafanyakazi**
***Lengo:*** Kukuza uchumi unaozingatia mazingira wenye usawa na thabiti.

**Uhifadhi wa Nishati ya Kibiashara na Nishati Mbadala**
***Lengo:*** Kupiga hatua kuelekea kuwa na majengo yasiyotoa kaboni yoyote na kusaidia katika kipindi cha mpito siyotoa kaboni.

**Mbinu za Kiasili za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi**
***Lengo:*** Kulinda mandhari safi, kurejesha mifumo ikolojia iliyoharibika na kuborsha ufikiaji sawa wa miundombinu inayozingatia mazingira, kivuli cha miti na maeneo ya umma yaliyotengwa kwa ajili mapumziko.

**Mifumo ya Kilimo na Chakula**
***Lengo:*** Kuza ufumbuzi wa mifumo ya kilimo na ya kuzalisha chakula.

**Kwa maelezo zaidi, tembelea erie.gov/climateaction.**

Kaunti ya Erie
MABADILIKO YA TABIANCHI

# Muhtasari

## Rasimu ya Mpango wa Mikakati ya Jamii ya Kukabili Mabadiliko ya Tabianchi (Community Climate Action Plan)

Matokeo ya mabadiliko ya tabianchi yanatuzunguka kwa kila pande. Halijoto ya juu zaidi ya ziwa inasababisha dhoruba kali zaidi huku kasi ya juu ya upepo, mienendo ya maji inayosababishwa na mabadiliko ya shinikizo la anga na halijoto kali zinazidi kuwa mambo ya kawaida. Katika mwaka wa 2022, Marekani ilikumbwa na majanga yanayotokana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabia nchi ya kiwango cha dola bilioni 165, ikiwa ni kiwango cha tatu kwa ukubwa kuwahi kutokea.[1] Kaunti ya Erie, kama ulimwengu wote, inakabiliwa na tishio la kukumbwa na hali ya dharura inayotokana na mabadiliko ya tabianchi, ambayo inaongezea kwa changamoto za muda mrefu za ukosefu wa usawa wa kiuchumi na dhuluma kwa misingi ya rangi.



Ripoti ya hivi karibuni zaidi ya Jopo la Serikali Mbalimbali kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (IPCC), tathmini ya kimataifa ya kisayansi kuhusu vitisho vinavyotokana na mabadiliko ya tabianchi, ilitolewa mwaka 2022 na inaonyesha kuwa kipindi cha muda wa kuchukua hatua na kupunguza ukubwa wa athari za mabadiliko ya tabianchi kinaendelea kupungua.[2]

Lakini kuna mambo mengi ya kukuwa na matumaini juu yake. Kaunti ya Eriepeke yake haiwezi kuzuia mabadiliko ya tabianchi, lakini uchukuaji wa hatua na usaidizi kutoka kwa serikali ya jimbo, serikali kuu na serikali ya mitaa serikali, pamoja na wakazi wa jamii na wafanyabiashara wa biashara za eneo la Kaunti ya Erie na kote ulimwenguni, wanaweza kutoa mchango mkubwa katika kupunguza utoaji wa hewa chafu (Greenhouse Gases, GHG) duniani kote.Kwa sababu athari za mabadiliko yatabianchi tayari zinashuhudiwa, ni sharti pia tujiandae kustahimili athari za sasa na zijazo.

**Mpango wa Mikakati ya Jamii ya Kukabili Mabadiliko ya Tabianchi (Community Climate Action Plan - CCAP) unalenga kuunda fursa za kushughulikia mabadiliko ya tabianchi huku pia ukilinda wakazi wetu, ikibuni nafasi za kazi, ikilinda mashamba yenye tija na kushughulikia masuala ya ukosefu wa usawa. Mpango huu unataja malengo, mikakati na hatua ambazo Kaunti inaweza kuchukua, iwe ni kwa njia ya moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja ili kushughulikia suala hili muhimu.**

Ili kushughulikia vyema suala la mabadiliko ya tabianchi na kupunguza utoaji wa gesi ya GHG katika jamii, Kaunti ilitisha mkutano wa Kikosi Kazi cha Jamii kinachoshighulikia masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi ili kishauri Kaunti na kuanza mchakato wa kupanga kuunda mpango wa CCAP hii inayozingatia usawa.

Kikosi Kazi hicho kilibaini mada kumi na kikaunda vikundi vya kazi vya wataalamu mbalimbali ili kuunda vitengo vya kushughulikia mpango wa mada hizi. Kati ya mwezi Machi mwaka wa 2020 na mwezi Februari mwaka wa 2023, Kaunti ya Erie iliratibu uundaji wa mpango wa CCAP pamoja na wafanyakazi wa kujitolea zaidi ya 100 kutoka Kikosi Kazi na jamii.

[1] https://www.ncei.noaa.gov/access/billions/

[2] https://www.ipcc.ch/report/ar6/wg2/


Sura hizo ziliandikwa ili kujumuisha malengo, mikakati, na vipengee vya vitendo vinavyoonekana ambavyo Kaunti ya Erie inaweza kuchukua ili kupunguza utoaji wa gesi ya GHG na kuifanya jamii kustahimili mabadiliko ya tabianchi. Tovuti ya, www.erie.gov/climateaction, iliundwa ili kuhifadhi hati kwa ajili ya umma kutoa maoni na pia kuwasiliana namna wanajamii wanavyoweza kuhusika.

## Mipango ya Kikanda na Majimbo

Mpango huu unategemea misingi ya mipango ya awali ya kikanda, kama vile Mpango Endelevu wa Kanda ya Western New York (WNY) (2013)[3] na **JUHUDI YA KUENDELEZA ENEO (One Region Forward)**. Muda mfupi baada ya Kikosi Kazi kuanza kukutana mwaka wa 2019, Sheria ya Uongozi wa Mashirika Yanayoshughulikia Mabadiliko ya Tabianchi ya New York na Usalama wa Jamii (CLCPA) ilipitishwa. Ingawa, mpango wa Kaunti ya Erie unatofautiana na mpango wa jimbo, mpango wa jimbo unaweza kusababisha kutokea kwa fursa za ufadhili na ulizingatiwa kwa uangalifu.

## Kujitolea Kuhakikisha kuwa kuna Usawa

Tatizo kuu la ukosefu wa usawa ambalo limerithiwa kutoka vizazi vilivyotangulia bado upo leo katika Kaunti ya Erie vilevile kote nchini. **Kaunti ya Erie imeangazia Mpango huu kwa kujitolea kutumia mtazamo wa usawa wakati wa kuunda mikakati ya Mpango na vipengee vya hatua za mpango**. Maelezo zaidi kuhusu mada hii yanaweza kupatikana katika Sura ya 2: Haki Inayohusiana na Masuala ya Tabianchi.





## Zana Zinazotumiwa na Serikali ya Kaunti ya Erie

Ingawa Kaunti ya Erie ina wakazi wengi kuliko baadhi ya nchi na inadhibiti barabara nyingi kuliko baadhi ya majimbo, jukumu la Kaunti ya Erie ni ndogo zaidi kuliko jukumu la serikali kuu au serikali ya jimbo. Majukumu mengi ya Kaunti ya Erie ni pamoja na kutoa huduma za kijamii na mipango ya afya ya umma, kuratibu huduma za hali ya dharura, pamoja na kudumisha miundombinu muhimu. Kwa hivyo, kulinda jamii yetu na haswa wakazi walio hatarini kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi ni jukumu la kiasilia kwa Kaunti. Kaunti ya Erie pia inaweza kupanua mipango hii ili kusaidia manispaa na kaya katika juhudi zao za kupunguza uzalishaji wa gesi ya GHG na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Iwapo Kaunti ya Erie haiwezi kuwa na mamlaka ya kudhibiti au kutekeleza hatua moja kwa moja, ina uwezo wa kutetea na kuongoza.

## Manufaa kwa Afya ya Umma

Afya ya umma na mabadiliko ya tabianchi zmeunganishwa kwa kina. Magonjwa ya kiafya yanayotokana na hewa chafu, maji chafu na matukio yanayotokana na hali mbaya ya hewa yanaweka shinikizo kwa wale ambao tayari wanatatizika na magonjwa ya mishipa ya moyo, matatizo ya kupumua na matatizo mengine ya kiafya. Matatizo ya kiafya yanayoendelea pamoja na majengo ya zamani ya Kaunti ya Erie huongeza tishio la afya ya umma kuwepo kwa joto na baridi kali, haswa kwa watu wetu walio hatarini zaidi, watoto na wazee, katika jamii ambazo huwa tofauti nyingi za kiafya na ukosefu wa usawa.

## Utekelezaji

Utekelezaji wa mpango huu utahitaji mtazamo wa pande nyingi, ikiwa ni pamoja na kushirikiana na jamii yetu, kupata vyanzo vya ufadhili vya jimbo na serikali kuu na kuimarisha ushirikiano.

Kubuni mipango inayowasilisha hatua ambazo tunaweza kuchukua kama jamii ili kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, huku kwa wakati huo huo tukijitayarisha kwa ajili ya athari za mabadiliko ya hali ya hewa, ni muhimu kwa sura zote ndani ya Mpango huu. Ukuzaji wa elimu na ufikiaji sharti pia kuhakikishe kuwa tunajaribu kuwafikia wakazi wote kwa kuzingatia ufikiaji, usambazaji, tafsiri, masuala ya ufikiaji, na zaidi. Itakuwa muhimu kwa Kaunti kusaidia jamii yetu kufahamu fursa za kupunguza utoaji wa gesi ya GHG na kubadikia kulingana na mabadiliko ya tabianchi ili kutimiza mengi ya malengo, mikakati, na hatua zilizoainishwa katika Mpango huu.




Kaunti ya Erie itahitaji kutafuta njia za kuunganisha rasilimali za kifedha na kutumia mipango ya ufadhili ya serikali ya jimbo na serikali kuu ili kushughulikia mabadiliko ya tabianchi. Sheria za serikali ya jimbo na serikali kuu zilizopitishwa hivi majuzi, kama vile Sheria ya Dhamana ya Mazingira na Sheria ya Kupunguza Mfumuko wa Bei, zitakuwa vyanzo muhimu vya ufadhili.




**Kama vile Mpango huu ulihusisha kazi ya washirika kote katika jamii, Kaunti ya Erie haitaweza kufikia malengo ya Mpango huu peke yake. Kaunti ya Erie itahitaji kufanya kazi na manispaa, wilaya za shule, biashara, mashirika yasiyo ya faida, vikundi vya jamii na wakazi ili kutimiza uwezo wake wote.**

## Shukrani

Juhudi hizi zilifanywa bila ya usaidizi wa mshauri wakiufundi na ilitegemea juhudi za washikadau wa kujitolea na wafanyakazi wa Kaunti. Kaunti inatoa shukranikwa mwenyekiti wa Kikosi Kazi, Dkt. Susan Clark, Viongozi wetu wa Kikundi Kazi na washiriki wetu wengi wa washikadau ambao walijitolea uongozi na utaalam wao na wakasaidia sana katika kufanikisha mradi huu. Wafanyakazi walifadhiliwa kwa sehemu na Idara ya Uhifadhi wa Mazingira ya Jimbo la New York (NYS).

## Hatua Zinazofuata

Utekelezaji wa Mpango wa Mikakati ya Jamii ya Kukabili Mabadiliko ya Tabianchi (Community Climate Action Plan) umeanza. Mpango wote wa CCAP unapatikana katika www.erie.gov/climate-action. Unahimizwa kutoa maoni katika sustainability@erie.gov.

[3] https://regional-institute.buffalo.edu/wp-content/uploads/sites/155/2020/10/Western-New-York-Regional-Sustainability-Plan.pdf